NORTH Dakota | Health
Be Legendary.™

☑ Kuendelea Kupata Habari kuhusu Chanjo za COVID-19

CDC inapendekeza kwamba watu waendelee kupata habari kuhusu chanjo zao za COVID-19, ikiwemo dozi za ziada kwa watu ambao kingamaradhi imeathirika au dozi za kiongeza nguvu mara kwa mara. Watu ambao kingamaradhi yao imeathirika kidogo au vibaya zaidi wanapaswa kupata chanjo ya msingi ya ziada na chanjo ya kiongeza nguvu.

Je, ni nani anayestahiki kupata chanjo za COVID-19?

Watu wote walio na miaka 5 na zaidi wanastahiki kupata mikondo ya msingi ya chanjo ya COVID-19 nchini Marekani. Vilevile, watu wote ambao kingamaradhi ao imeathirika kidogo hadi vibaya zaidi na wana miaka 5 na zaidi wanastahiki kupata dozi ya ziada (ya 3) ya chanjo ya COVID-19 pamoja na mikondo yao ya msingi.

Kuanzia tarehe 5 Januari, 2021, watu wote walio na miaka 12 na zaidi ambao wamekamilisha mikondo yao ya msingi ya chanjo ya COVID-19 wanastahiki dozi ya kiuongeza nguvu pindi tu wanapofikisha kipindi cha kutegemea wakati kwenye mikondo ya msingi waliyopata.

Je, chanjo gani za COVID-19 zinapendekezwa?

CDC inapendekeza kwamba watu wote wapate mikongo ya msingi na dozi ya kiongeza nguvu ya chanjo ya mRNA (Pfizer au Moderna) COVID-19. Watu walio na miaka 18 na zaidi waliopata dozi ya msingi ya Janssen (Johnson & Johnson) wanapendekezwa kupata dozi ya kiongeza nguvu ya chanjo ya mRNA miezi miwili baada ya dozi yao ya msingi.

Tafadhali zungumza na mtoa huduma wako wa afya ili kuamua chanjo ya COVID-19 inayokufaa.

Je, ni nani anayesemekana kuwa na kingamaradhi iliyoathirika?

Watu wanasemekana kuwa na kingamaradi iliyoathirika kidogo au vibaya zaidi ikiwa:

- Wamekuwa wakipata tiba ya saratani ya vivimbe au saratani za damu
- Wamepata upandikizaji wa kiungo na wanakunywa dawa ya kukandamiza mfumo wa kingamaradhi
- Wamepata upandikizaji wa seli ya shina ndani ya miaka miwili iliyopita au wanakunywa dawa ili kukandamiza mfumo wa kingamaradhi
- Upungufu wa kingamaradhi ya msingi kidogo au mbaya zaidi (kama vile dalili ya DiGeorge, dalili ya Wiskott-Aldrich)
- Wana maambukizi ya juu au yasiyotibiwa ya VVU
- Tiba ya mara kwa mara kwa kutumia corticosteroid za dozi ya juu au dawa nyingine inaweza kukandamiza mkabiliano wa kingamaradhi

Watu wanapaswa kuzungumza na mtoa huduma wao wa afya kuhusu hali yao ya afya na ikiwa kupata chanjo ya msingi ya ziada kunawafaa.

NORTH Dakota | Health
Be Legendary.™

Kuendelea Kupata Habari: Watoto wa Miaka 5-11

Mikondo ya Msingi:
Watoto wote wa miaka 5-11 wanastahiki mikondo ya msingi ya dozi mbili za chanjo ya Pfizer-BioNTech COVID-19 iliyotengwa kwa angalau umbali wa siku 21. Vilevile, watoto wote wa miaka 5-11 walio na kingamaradhi iliyoathirika kidogo au vibaya zaidi wanastahiki dozi ya ziada (ya 3) pamoja na mikondo yao ya msingi iliyotengwa kwa siku 28 baada ya dozi yao ya pili.
Dozi ya Kiongeza Nguvu:
Watoto wa miaka 5-11 kwa sasa hawastahiki dozi ya kiongeza nguvu ya COVID-19.

Kuendelea Kupata Habari: Vijana wa miaka 12-17

Mikondo ya Msingi:
Vijana wote wa miaka 12-17 wanastahiki mikondo ya msingi ya dozi mbili za chanjo ya Pfizer-BioNTech COVID-19 iliyotengwa kwa angalau umbali wa siku 21. Vilevile, watoto wote wa miaka 12-17 walio na kingamaradhi iliyoathirika kidogo au vibaya zaidi wanastahiki dozi ya ziada (ya 3) pamoja na mikondo yao ya msingi iliyotengwa kwa siku 28 baada ya dozi yao ya pili.
Dozi ya Kiongeza Nguvu:
Vijana wa miaka 12-17, ikiwemo wale ambao kingamaradhi imeathirika, wanastahiki dozi ya kiongeza nguvu ya Pfizer COVID-19 miezi mitano baada ya kukamilisha mikondo yao ya msingi.

Kuendelea Kupata Habari: Watu wazima wa zaidi ya miaka 18

Kwa wale waliopata Mikondo ya Msingi ya Pfizer

Mikondo ya Msingi:
Watu wazima wote wa miaka 18- na zaidi wanastahiki mikondo ya msingi ya dozi mbili za chanjo ya Pfizer-BioNTech COVID-19 iliyotengwa kwa angalau umbali wa siku 21. Vilevile, watu wote wa miaka 18 walio na kingamaradhi iliyoathirika kidogo au vibaya zaidi wanastahiki dozi ya ziada (ya 3) pamoja na mikondo yao ya msingi iliyotengwa kwa siku 28 baada ya dozi yao ya pili.
Dozi ya Kiongeza Nguvu:
Watu wazima wa miaka 18, ikiwemo wale ambao kingamaradhi imeathirika, wanastahiki dozi ya kiongeza nguvu ya COVID-19* baada ya kukamilisha mikondo yao ya msingi.

*Ingawa chanjo za mRNA zinapendelewa, chanjo ya Johnson & Johnson COVID-19 zinaweza kuzingatiwa katika hali fulani.

Kuendelea Kupata Habari: Watu wazima wa zaidi ya miaka 18
kwa wale waliopata Mikondo ya Msingi ya Moderna

Mikondo ya Msingi:
Watu wazima wote wa miaka 18- na zaidi wanastahiki mikondo ya msingi ya dozi mbili za chanjo ya Moderna COVID-19 iliyotengwa kwa angalau umbali wa siku 28. Vilevile, watu wote wa miaka 18 walio na kingamaradhi iliyoathirika kidogo au vibaya zaidi wanastahiki dozi ya ziada (ya 3) pamoja na mikondo yao ya msingi iliyotengwa kwa siku 28 baada ya dozi yao ya pili.
Dozi ya Kiongeza Nguvu:
Watu wazima wa miaka 18, ikiwemo wale ambao kingamaradhi imeathirika, wanastahiki dozi ya kiongeza nguvu ya COVID-19* baada ya kukamilisha mikondo yao ya msingi.

*Ingawa chanjo za mRNA zinapendelewa, chanjo ya Johnson & Johnson COVID-19 zinaweza kuzingatiwa katika hali fulani.

Kuendelea Kupata Habari: Watu wazima wa zaidi ya miaka 18
kwa wale waliopata Mikondo ya Msingi ya Johnson & Johnson

Dozi ya Msingi:
Watu wazima wote wa miaka 18 na zaidi wanastahiki mkondo wa msingi wa dozi moja ya chanjo ya Johnson & Johnson* COVID-19. Watu wazima ambao kingamaradhi yao imeathirika kidogo hadi vibaya zaidi walio na miaka 18 na zaidi ambao wamepata dozi ya Johnson & Johnson HAWASTAHIKI dozi ya ziada (ya 2).
Dozi ya Kiongeza Nguvu:
Watu wazima wa miaka 18, ikiwemo wale ambao kingamaradhi imeathirika, wanastahiki dozi ya kiongeza nguvu ya COVID-19* miezi miwili baada ya kukamilisha mikondo yao ya msingi.

*Ingawa chanjo za mRNA zinapendelewa, chanjo ya Johnson & Johnson COVID-19 zinaweza kuzingatiwa katika hali fulani.

Mahali pa Kuchanjwa

Maelezo kuhusu watoa huduma wa chanjo ya COVID-19 na kliniki zilizo karibu nawe zinaweza kupatikana kwenye ukurasa wa NDDoH COVID Vaccine Locator. Pia unaweza kuwasiliana na NDDoH Hotline kwa nambari 1.866.207.2880 kwa usaidizi.